MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Cheche za Fikra

JUZUU 2 TOLEO 4

SEPTEMBA 23, 2008

KIJARIDA CHA BURE— UKISHASOMA MPE MWINGINE—USIBANIE!

LOWASSA KUFANYWA ZUMA WA TZ?



Aliyekuwa Waziri Mkuu Lowassa akiwa kwenye ziara

Na. Fred Katunzi



Baada ya aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano Mhe. Edward Lowassa kujiuzulu kufuatia kashfa ya Richmond na baada ya ofisi yake kuhusishwa na uzembe uliosababishia Taifa hasara kubwa kwa kuingia mkataba na kampuni hewa, kumekuwa na dalili za kujaribu kumsafisha.
Mara tu baada ya kuachia ngazi kwa mtindo wa kususa Waziri Mkuu aliyejiuzulu alijaribu kujisafisha kwa kutumia TVT (siku hizi TBC) kwa kufanya mahojiano ambayo yalikatishwa hewani.

Wakati ule Mwanakijiji alitoa ripoti ya kwanza na ya pekee juu ya mpango wa kumrejesha Lowassa madarakani kwa kuanza kumsafisha kwenye vyombo vya habari na katika sehemu mbalimbali.

Mpango huo ulijulikana kama Agenda 21

Mpango huo ulijulikana kama Agenda 21.

Katika taarifa yake hiyo Ndg. Mwanakijiji alisema hivi tarehe 22 Februari 2008 kuhusu mtandao huo ulioundwa, "mtandao huo ambao siyo tu una lengo la kujibu mapigo lakini pia umedhamiria kurejesha na kuinua tena wasifu wa aliyekuwa Waziri Mkuu Bw. Edward Lowassa."

Katika taarifa yake hiyo Bw. Mwanakijiji alilitahadharisha Taifa kuhusu mtandao huu kuwa "mtandao huo unaundwa na wanasiasa wa chama tawala ambao wamejikuta hawamo tena serikalini, wafanyabiashara maarufu, vyombo kadhaa vya habari (ambavyo vingine vimeanza kuandika habari zinazotokana na "agenda" hiyo) na mashabiki wengine wakubwa wa aliyekuwa Waziri Mkuu."

Kwa miezi karibu saba sasa tangu taarifa hizo za awali zitolewa inaonekana juhudi za mtandao huo hazijakoma na zinaendelea.
(inaendelea Uk 2)



Benjamin. G. Mwalukasa
Mhariri

Kijarida Ulichoshika

- **Kinatoka kila Jumanne**
- **Ni cha bure kabisa!**
- **Kisichofungamana na chama chochote au fisadi yeyote!**
- **Kiko huru, kinathubutu, na hakiogopi mtu au hoja yoyote.**
- **Ni kijarida chako!**
- **Haki zote za kuchapa na kunakili zimeruhusiwa!**

HOJA YA MWANAKIJIJI — TUKIJIAMINI, TUNAWEZA

Hivi umewahi kujiuliza nchi za "wazungu" zimefikaje zilipofika? Je umewahi kujiuliza huko "Ulaya" wamewahi kuwa na maisha duni, ya kuishi kwenye nyumba za udongo au katika mazingira duni?

Hivi unafikiri Wazungu wamewahi kuishi katika jamii inayoua watu wanaodhaniwa kuwa ni wachawi?

Majibu kwa maswali hayo ni kuwa kama hujawahi basi ndiyo nakujulisha. Nchi za Ulaya na Marekani zimepitia katika mazingira magumu na duni kama ya kwetu.
Kiini cha mabadiliko yao ni ule moyo wa kukataa majibu mepesi, kujaribu vitu vipya na kutamani maisha bora na yaliyorahisishwa.

Na sisi tukitaka kujenga maisha mazuri ni lazima tuanze kujiamini kama mtu mmoja mmoja na kama taifa zima kuwa na sisi tunaweza Taifa la kisasa na lililoendelea kama yale ya Ulaya.
Tusikubali kujiona duni tena!

Ndani ya Toleo Hili

Lowassa kama Zuma?	1
Tukijiamini tunaweza	1
Vigogo wa Ufisadi —3	2
Habari kwa Ufupi	2
Walioghushi vyeti BoT	3
Ya Janet na Sophia	3
Picha, Katuni na Maoni	4

HABARI MBALIMBALI

VIGOGO WENGINE WA UFISADI

Na. Mahmoud Rashid



Katika sehemu hii ya tatu na ya mwisho ya vigogo wa ufisadi tutawaangalia watu wengine ambao majina yao yanatajwa sana katika mambo mbalimbali yanayohusiana na ufisadi.

Andrew Chenge: Huyu alikuwa ni Mwanasheria Mkuu na chini yake mikataba kadhaa mibovu kabisa kusainiwa katika historia ya nchi yetu ilisainiwa. Utajiri wake ni mkubwa kama ilivyooneshwa katika tuhuma zilizotangulia kujiuzulu kwake toka Uwaziri wa Miundo Mbinu.

Bw. Chenge amekuwa akichunguzwa na taasisi ya Uhalifu Mkubwa ya Uingereza kwa kuhisiwa kukatiwa karibu Shs. Bilioni moja katika sakata la ununuzi wa rada ya kijeshi, manunuzi ambayo yalimhusisha Bw. Saileth Vithlani tuliyemuangalia katika toleo la nne.

Pamoja na kashfa zilizomzunguka chama chake bado kinamtegemea katika mambo ya maadili ya uongozi kinyume cha matarajio ya watu wengi.

Bernard Mchomvu: Huyu bwana anadaiwa kuhusika katika ununuzi wa boti za jeshi ambazo hazikuwa zinafanya kazi ipasavyo licha ya kudaiwa kuwa ni mpya.

Alikuwa ni Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na ndiye aliyehusika na manunuzi ya malori ya IVECO yakiwahusisha marafiki zake Vithlani na Somaiya. Malori ambayo inadaiwa yaligharibu karibu mara mbili ya bei yake kamili.

Bw. Mchomvu anadaiwa kupata gawio nono tu kutokana na "dili" la rada yeye na wenzake.

Sir. Andy Chande: Kati ya Watanzania wote ambao wanaonekana kuwa na nguvu ya ajabu ya kufanya mambo yatendeke ni Bw. Andy Chande ambaye ni rafiki wa karibu wa Rais Mkapa.

Akitumia mtandao wa "Waashi" (Free Masons) ameweza kuwaleta karibu yake viongozi wengi mbalimbali na ambao kiu yao ya utajiri haijatoshelezwa.

Kwa baadhi ya watu Sir. Andy ndiye baba wa tabia za kifisadi akiwa anaishawishi serikali kutoa mikataba kwa makampu kadhaa ya kiasia ukiwemo mkataba wa Ubinafsishaji wa shirika la reli.

Yeye ni rafiki wa karibu (na inadaiwa kuna undugu) na vigogo wengine wa ufisadi nchini Bw. Saileth Vithlani na Tanil Somaiya.

Bw. Chande amekuwemo katika siasa za

UKIMALIZA KUSOMA MPATIE MWINGINE BURE!

Akitumia mtandao wa Waashi (Free Masons)



Afrika ya Mashariki na hasa Tanzania kwa muda mrefu na hakuna lolote ambalo linaweza kufanyika katika miradi mikubwa bila yeye au "watu wake" kujua au kuhusishwa.

Pichani Sir Andy Chande akiwa amevalia mavazi ya cheo chake katika Kundi la Waashi analoliongoza katika eneo letu la Africa ya Mashariki na Seychelles.

Haijulikani ni kwanini hadi hivi sasa Sir. Andy Chande hajajitokeza kukemea vitendo vya ufisadi nchini kwa kauli kali zaidi.

LOWASSA (KUTOKA 1)

Hata hivyo sasa hivi mtandao huo unajaribu kutengeneza mazingira kama ya Zuma. Kuna dalili ambazo tutaziona siku si nyingi za jinsi gani kundi la mtandao huu linavyojaribu kwa kila hali kuonekana linawatetea wale walioangushwa kutokana na tuhuma za ufisadi.

Kijarida hiki cha "Cheche" kitaendelea kukuletea na kukutahadharisha juu ya juhudi zao hizo. Mojawapo ya juhudi ambayo wameanza kuitumia sasa ni matumizi ya simu za mkononi kutishia watu mbalimbali wakiwemo wanasiasa na wafanyabiashara na waandishi.

Kutokana na uwezo mdogo wa Polisi na ulaini wa sheria zetu kuna uwezekano kundi hili likafanikiwa katika mipango yao ya kumfanya Lowassa aonekane kama mtu aliyeonewa na hivyo kujaribu kuleta kama yaliyomkuta Rais Mbeki siku ya Jumapili alipolazimishwa kujiuzulu kutokana na nguvu za mpinzani wake ndani ya ANC Bw. Jacob Zuma.

Wiki ijayo tutakuletea taarifa ya jinsi gani usalama wa Taifa unatishiwa na uwezo wa kundi hili na harakati zake za kujita-

HABARI KWA UFUPI

New York, NY

Rais Kikwete ameondoka nchini mwishoni mwa Juma kuelekea Marekani ambako akiwa huko atalihubua Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa siku ya Jumanne.

Pamoja na hayo Rais Kikwete anatarajiwa kushiriki katika mikutano na mazungumzo na viongozi mbalimbali pamoja na taasisi mbalimbali za maendeleo.

Katika ziara hiyo Rais Kikwete pia ataungana na mke wake Bi. Salma Kikwete aliyetangulia nchini humo Jumapili iliyopita kwa uangalizi wa afya yake.

Rais Kikwete anatarajiwa pia kuchunguzwa afya akiwa nchini humo.

NGUVU ZA HOJA

YASIISHIE KWA WALIOGHUSHI

Na. B. Mwalukasa

Mojawapo ya vitu ambavyo viliibuka kufuatia kashfa ya EPA na wizi wa Benki Kuu ni kugundulika kwa kujazana kwa watoto wa wakubwa mbalimbali kwenye taasisi hiyo nyeti kiasi cha kusababisha maswali kuulizwa.

Idara hiyo imedaiwa kuajiri watoto wengi wa viongozi mbalimbali kiasi kwamba watu wanaamini kuwa kuna dalili ya ufisadi wa aina fulani, upendeleo wa kifamimilia nepotism) au kile ambacho Baba wa Taifa alikiita kuwa ni "undugunization".

Baadhi ya watoto hao ni Pamella Lowassa, Filbert Frederick Sumaye, Zalia Kawawa, Harieth Lumbanga,Salama Ally Mwinyi, Rachael Muganda, Sylvia Omari Mahita, Justina James Mungai, Kenneth John Nchimbi, na Blassia Blassius William Mkapa. Wengine ni Violeth Phillemon Luhanjo,Liku Irene Katte Kamba, Thomas Mongella,Allen Shibuda, na Jabir Abdallah Kigoda.

Tuhuma zilizotolewa ni kuwa watoto hao wamepata nafasi hizo kwa upendeleo wa aina fulani kutokana na nyadhifa za wazazi wao serikalini. Na kwa vile kuna matukio mengi ya kifisadi yanayohusu Benki Kuu basi kuna imani kuwa watoto hao wasingeweza kuumbua mambo ambayo yangewaharibia wazazi wao kazi.

Sasa hatua zilizochukuliwa mwishoni mwa juma za kuwafungulia mashtaka wale ambao wanatuhumiwa kugushi vyeti na kuweza kupata ajira Benki Kuu ni hatua za kupongezwa na kuungwa mkono.

Hata hivyo, hatua hizo zisiishie kwa hawa na wenye kugushi tu; bali zifike hadi kwa wale ambao wamejipachika udaktari wa kughushi au kudai kuwa wana elimu fulani ambayo hawana.

Ni kwa sababu hiyo basi tunaamini kuwa suala la kufuatilia elimu lisiishie kwa watumishi hawa tu bali pia kwa wanasiasa ambao wanashika madaraka mbalimbali katika serikali yetu.

Pamoja nao ni wale wanaojiita madaktari waliopata udaktari wao kutoka katika vyuo ambavyo havitambuliwi kutoa elimu hiyo na taasisi zinazosimamia elimu hiyo kwenye nchi zao.

Miongoni mwao ni pamja na Naibu wa Ulinzi na Kujenga Taifa Mhe. Emmanuel Nchimbi (anayejiita ni Dr" na pia Mhe. Mary Nagu ambaye naye anajiita ni "Dr". Na mwingine ni Waziri wa Fedha Bw. Mustafa Mkullo.

Hawa na wengine wengi ambao wanajulikana katika nafasi mbalimbali za serikali na vyuo vikuu (kuna wengi wamejazana pale Mzumbe) watakiwe kuachana na kujitangaza kuwa wana elimu kutoka kwenye vyuo vinavyojulikana kama "Diploma mills".

Orodha ya vyuo ambavyo Wizara ya Elimu ya Juu haivitambui ipo; wakati umefika wa hatua kuanza kuchukuliwa siyo kwa kuwafikisha mahakamani hawa peke yao bali pia kuwavua nafasi viongozi wote ambao wamejivika udaktari wa kughushi na kuweza kujipatia nafasi mbalimbali za madaraka

Tukifanya hivyo tutakuwa tunawatendea haki wale wote waliohangaika kwenda shule na kusota kupata elimu ya juu.

Soma bure

jiko yao.

Inasikitisha Waziri mzima wa "Utawala" bora ameshindwa kutawala hisia zake na pia mama mzima na heshima zake kutokuonesha busara ya ukimya.

Tunapotaka nafasi hizi za uongozi tuwe tayari kulipa gharama yake ya kuwa tofauti na kuonesha mwenendo mzuri.

Sijui Rais Kikwete ataendelea kuvumilia tabia hii ya watu kudhalilisha ofisi na vyeo vyao mpaka lini? Tutaona kwenye kura.

YA JANETI NA SOPHIA— TUTAFIKA?

Na. Jessy L. Fundi



Malumbano ya viongozi wawili ambapo mmoja wao ana nafasi nyeti nchini yameniumiza kichwa, kunisikitisha na kunifanya nijisikie vibaya.

Inakuwaje kina mama wawili wenye heshima zao na ambao wanachukuliwa kama viongozi walumbane na kutoleana shutma kama mabinti walioko sekondari au wanaogombania bwana? Sielewi.

Vyovyote vile malumbano kati ya Waziri wa Nchi ofisi ya Rais anayeshughulikia Utawala Bora Bi. Sophia Simba na mama Janeti Kahama mke wa kiongozi maarufu nchini ni ya kusikitisha na yanaleta mfano mbaya kabisa kwa watoto wa kike, kina dada na kina mama wanaofikiria kugombea au kutafuta nafasi ya uongozi wa kisiasa.

Habari za mwanzo zilizotolewa na gazeti moja nchi zilionesha kuwa kulikuwa na majibizano ya aina fulani kati ya kina mama hawa wawili wakati wa mchakato wao wa kumtafuta Mwenyekiti mpya wa Jumuiya ya kina mama wa CCM. Hilo peke yake lingetosha.

Lakini halikutosha kwani baadaye mmoja wao (mama Kahama) alizungumza na chombo kimoja cha habari na kudai kuwa kilichotokea siyo tu malumbano bali ilifikia mahali kuwa Waziri Simba alijaribu kumpiga ngumi na alianguka kiasi cha "kudakwa" na watu asiowakumbuka.

Baadaye Waziri Simba akajitokeza na kukanusha hayo yote na kudai kuwa kuna wivu na ya kuwa kuna watu (bila ya shaka akimaanisha mama Kahama) hawapendi awe Waziri. Lakini kilichonikera ni pale katika utetezi wake alipoamua kukanusha kuwa ametumwa na Rais Kikwete kugombea nafasi hiyo ya Uenyekiti wa Jumuiya hiyo.

Ninachotaka kusema ni kuwa tabia waliyoionesha ni ya kitoto, na inayopakana kabisa na tabia za kishangingi na za mabinti walevi wasio na nyumba zao na ambao hawastahili kuongoza kitu chochote hata ma-

MOTO WA MABADILIKO UMEANZA...

Picha ya Wiki



Wanafunzi wakijiandaa kufanya mtihani wa STD VII



KATUNI ZA WIKI



K U T O K A K W E N Y E M T A N D A O

Amakweli sasa CCM imefilisika, tulifikiri wanashughuliia mafisadi wa pesa, kumbe wanaogopa kuwagusa vigogo wanakimbilia kushughulika na vihiyo, wapi na wapi? Watanzania hakika tunadanganywa. Hii yote ni kutaka kuwakingia kifua vigogo. Kweli serikali yetu imefikia hatua mbaya sana. Mungu ibariki Tanzania.—**Pd. Mapunda**

Nasikitisha,watu mlioaminiwa na Rais-mumsaidie kazi mnazozana kisa ulafi wa madaraka, jamii iwaelewe vipi? inaelekea wote wawili mmekosa busara na hamfai kuongoza jamii ikiwemo hiyo jumuiya ya umoja wa wanawake, nawashauri mjiuzulu nafasi mlizonazo sasa kwakuwa wote mmekosa uvumilivu; habari ndio hiyo—**Zizu S Zizu**

Nyinyi kina mama Kahama na Simba tayari mmeshaonesha tabia mbaya, hamfai kuiongoza UWT. Mtakiharibu chama; yaani mnaleta *kitchen party* katika chama. Majina yao yasipitishwe. Wakina Mamuya wapo na hao wengine wapewe nafasi.— **Lisa**

Namuunga mkono Mhe. Mbowe, watu wanatakiwa kujua kwamba huu ni wakati wa mabadiliko. Hao wanaosema CCM ni chama kitakacholeta maendeleo, ndio waliopewa vikofia na vikhanga. Na kauli mbiu ya kikwete, maisha bora kwa kila Mtanzania, ni hivyo vikofia vya yeboyebo.— **Othman Miraji**

Ukweli unauma eh?CCM itashinda (Tarime) habari ndiyo hiyo.—**Dino**

Mnataka "wapinzani" waungane na nani? Mvungi au Mtikila?? Na Kuungana ndio nini? CUF na CHADEMA wameungana. Hao waliobaki hawakuambulia hata asilimia 1 ya kura. Waungane ili iweje? Vyama vingine mzigo tu hamna lolote si chochote. Labda wakaungane na wenzano CCM ndio itakuwa poa. —**Fimbo**

Naziagiza jumuiya zote (za CCM) zifuate kanuni na maadili ya jumuiya zao na ninawaonya wagombea wasijiingize katika kampeni za rushwa, vitisho na kuchafuana. Vitu hivi ni adui wa demokrasia— **John Chiligati**

Cheche za Fikra
Mchapishaji na Mhariri Mtendaji

M. M. Mwanakijiji

Timu ya Waandishi
Benjamin Mwalukasa— Mhariri

Freddy Katunzi—Habari za Siasa

Mahmoud Rashid—Habari mbalimbali

Jessica L. Fundi – Makala

Kwa kujiandikisha,
maoni, habari, na ushauri

Tuandikie: Mhariri@klhnews.com

Tembelea: http://www.klhnews.com

Kanusho: ***Mawazo yanayonukuliwa hayawakilishi msimamo au mawazo ya mchapishaji na utawala wa kijarida hiki.***